## SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAFIRI BARABARANI NAM. 7 YA MWAKA 2003

---

### MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza Kutumika.

2. Kusomwa.

**SEHEMU YA PILI**
**VIFUNGU VYA MAREKEBISHO**

3. Marekebisho ya kifungu cha 2.

4. Marekebisho ya kifungu cha 4.

5. Kuongezwa kifungu kipya cha 4A.

6. Kuongezwa kifungu kipya cha 4B.

7. Kuongezwa kifungu kipya cha 4C.

8. Marekebisho ya kifungu cha 5.

9. Marekebisho ya kifungu cha 9.

10. Marekebisho ya kifungu cha 14.

11. Marekebisho ya kifungu cha 15.

12. Marekebisho ya kifungu cha 16.

13. Kuongezwa kifungu kipya cha 16A.

14. Kuongezwa kifungu kipya cha 16B.

15. Kuongezwa kifungu kipya cha 16C.

16. Kuongezwa kifungu kipya cha 16D.

17. Kuongezwa kifungu kipya cha 16E.

18. Kuongezwa kifungu kipya cha 16F.

19. Kuongezwa kifungu kipya cha 16G.

20. Kuongezwa kifungu kipya cha 16H.

21. Kuongezwa kifungu kipya cha 16I.

22. Kuongezwa kifungu kipya cha 16J.

23. Kuongezwa kifungu kipya cha 16K.

24. Kuongezwa kifungu kipya cha 16L

25. Marekebisho ya Kifungu cha 18.

26. Kuongezwa kifungu kipya cha 18A.

27. Kuongezwa sehemu mpya ya XA.

28. Kuongezwa vifungu vipya.

**SHERIA NAM. 10 YA 2019**

**NIMESAINI**

Ashein

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

31 Disemba, **2019**

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAFIRI BARABARANI NAM. 7 YA MWAKA 2003

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza Kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Barabarani, 2019 na itaanza kutumika mara tu baada ya kusainiwa na Rais.

Kusomwa.

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usafiri Barabarani Nam. 7 ya mwaka 2003 ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

## SEHEMU YA PILI
## VIFUNGU VYA MAREKEBISHO

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**3.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) Kufuta tafsiri ya neno "Mamlaka" na kuweka badala yake maneno kama ifuatavyo;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

(b) Kuongeza tafsiri mpya ya neno "Bodi " na kuweka badala yake maneno kama ifuatavyo :

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria hii:

(c) Kuingiza tafsiri ya neno jipya "Mkurugenzi Mkuu"kama ifuatavyo:

"Mkurugenzi Mkuu" ina maana kama inavyoelezwa chini kifungu cha 4A cha Sheria hii.

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**4.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa kifungu kipya cha 4 kama ifuatavyo :

Kuanzishwa kwa Mamlaka.

4.-(1) Kunaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ya Zanzibar.

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea, cha kudumu, chenye muhuri wake, na kwa jina lake kitaweza kufanya yafuatayo:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua au kuhaulisha mali inayohamishika na isiyohamishika;

(c) kuingia kwenye mikataba au miamala yoyote kwa mujibu wa sheria za Zanzibar;

(d) kukopa kiasi chochote cha fedha kutoka katika taasisi za fedha kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(e) kufanya au kutekeleza jambo lolote ambalo kisheria Mamlaka kwa asili yake, inaruhusika kufanya au kutekeleza.

Kuongeza kifungu kipya cha 4A.

**5.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 4A mara tu baada ya kifungu cha 4 kama ifuatavyo:

Mkurugenzi Mkuu.

**4A**.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu akiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza au kiwango kinacholingana na hicho katika fani ya uhandisi, usafirishaji, usalama barabarani, utawala wa biashara au sheria kutoka taasisi ya elimu ya juu inayotambulika; na

(c) ana uzoefu wa kazi angalau miaka kumi katika utumishi wa umma.

Kuongeza kifungu kipya cha 4B.

**6.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 4B mara tu baada ya kifungu cha 4A kama ifuatavyo:

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

**4B**.-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Mamlaka na atakuwa na dhamana za kila siku za uendeshaji, utekelezaji na usimamizi wa Mamlaka.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu atakuwa dhamana wa:

(a) kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya Mamlaka;

(b) kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha na mali za Mamlaka;

(c) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi wa Mamlaka;

(d) kushirikiana na taasisi nyengine na jumuiya mbalimbali zinazohusiana na sekta ya usafiri wa barabara;

(e) kupendekeza kwa Bodi muundo wa kitaasisi wa ndani ambao ni wa kiuchumi, kifanisi na usio na gharama;

(f) kupendekeza na kutekeleza Mpango Mkakati, Mpango wa Kibiashara na Mpango wa Uendeshaji wa Mamlaka;

(g) kuhakikisha kwamba sera za Mamlaka zinatekelezwa na kwamba malengo, shabaha na viwango vya huduma vilivyokubaliwa vinafikiwa;

(h) kutoa ushauri kwa Bodi kwa mambo yote yaliyo chini ya dhamana ya Mamlaka; na

(i) kutekeleza kazi nyengine yoyote ambayo ni ya lazima katika utekelezaji wa Sheria hii kama atavyopangiwa na Bodi.

(3) Mkurugenzi Mkuu, katika utekelezaji wa kazi zake, atawajibika kwa Bodi.

Kuongeza kifungu kipya cha 4C.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 4C mara tu baada ya kifungu cha 4B kama ifuatavyo:

Idara na Vitengo.

**4C.**-(1) Mamlaka inaweza kuanzisha Idara na Vitengo kama itakavyopendekezwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Wakuu wa Idara chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki watateuliwa na Waziri baada ya kupendekezwa na Bodi, na

(3) Wakuu wa vitengo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki watateuliwa na Bodi baada ya kupendekezwa na Mkurugenzi Mkuu.

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**8.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) Katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufutwa maneno "Msimamizi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Barabarani" na kuweka badala yake maneno "Mkurugenzi Mkuu". Maneno haya yatasomeka kila yatakapojitokeza katika Sheria Mama;

(b) kwa kufutwa kifungu kidogo cha (2).

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**9.** Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa maneno "katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii, Mamlaka inaweza" na kuweka badala yake maneno "Mamlaka itakuwa na uwezo wa".

Marekebisho ya kifungu cha 14.

**10.** Kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinafutwa na kuandikwa kifungu kipya cha 14 kama ifuatavyo:

Kunaanzishwa Bodi.

**14.**-(1) Kunaanzishwa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Mkurugenzi mwenye dhamana ya barabara;

(d) Mkurugenzi mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa;

(e) Mkuu wa Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani Zanzibar;

(f) Wawakilishi wawili kutoka Jumuiya ya Wasafirishaji, mmoja kutoka Jumuiya ya Wamiliki wa Vyombo vya Usafiri na mwengine kutoka Jumuiya ya Madereva.

(2) Ukiwaacha wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wa Bodi watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika.

(3) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi, ikiwa:

(a) ni mzanzibari;

(b) anayo angalau shahada ya kwanza au kiwango kinachofanana na hicho kutoka taasisi ya elimu ya juu inayotambulika; na

(c) ana uzoefu wa kazi wa usiopungua miaka kumi katika utumishi wa umma.

(4) Bodi itamteuwa mmoja miongoni mwa wajumbe wake kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Marekebisho ya kifungu cha 15.

**11.** Kifungu cha 15 cha Sheria Mama kinafutwa na kuandikwa kifungu kipya cha 15 kama ifuatavyo:

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**15.**-(a) Mwenyekiti wa Bodi atatumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka minne kuanzia siku ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine; na

(b) Wajumbe wengine wa Bodi, isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, isipokuwa kama uteuzi wao umefutwa au umemaliza kwa njia yoyote kuwa wajumbe, watatumikia nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**12.** Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinafutwa na kuandikwa kifungu kipya cha 16 kama ifuatavyo:

Vikao vya Bodi.

**16.**-(1) Bodi itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana wakati wowote itakapotokezea haja katika kutekeleza kazi zake mahala ambapo Bodi itaamua ndani ya Zanzibar.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaongozwa na Mwenyekiti au kama hayupo na Makamu Mwenyekiti, endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliohudhuria kikao watamteua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao na mjumbe aliyeteuliwa kuongoza kikao atakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu ya Mwenyekiti ya uendeshaji wa vikao.

(3) Zaidi ya nusu ya wajumbe wa Bodi wataunda akidi ya kikao.

(4) Bodi itafanya maamuzi kwa kukubaliana, na ikitokezea kutokubaliana, maamuzi yatafikiwa kwa kupiga kura na ikitokezea kura kuwa sawa, Mwenyekiti au mjumbe anayeongoza kikao atakuwa na kura ya maamuzi.

(5) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, maamuzi yanaweza kufanywa na Bodi kwa kugawa karatasi kwa wajumbe waliopo Zanzibar kwa wakati huo lakini wasiopungua wajumbe watano ambapo kila mjumbe atatoa mawazo yake kwa maandishi .

(6) Azimio la maandishi lililotiwa saini na wajumbe wote chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, litakuwa na nguvu sawa kama uamuzi uliofanywa katika kikao cha kawaida.

Kuongeza kifungu kipya cha 16A.

**13.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16A mara tu baada ya kifungu cha16 kama ifuatavyo:

Mualikwa.

**16A.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria kikao chochote cha Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kuongeza kifungu kipya cha 16B.

**14.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16B mara tu baada ya kifungu cha16A kama ifuatavyo:

Kumbukumbu za Vikao vya Bodi

**16B.** Kumbukumbu za vikao vya Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na zitawekwa saini na Mwenyekiti wa kikao na Katibu wa Bodi.

Kuongeza kifungu kipya cha 16C.

**15.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16C mara tu baada ya kifungu cha16B kama ifuatavyo:

Mjumbe kutangaza maslahi.

**16C.** Mjumbe ambaye maslahi, ama moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja katika mkataba au mkataba unaopendekezwa au jambo lolote litakaloamuliwa na Bodi, atalazimika kutangaza aina ya maslahi yake kwa Bodi na mjumbe huyo hatashiriki katika uamuzi wa jambo hilo.

Kuongeza kifungu kipya cha 16D.

**16.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16D mara tu baada ya kifungu cha16C kama ifuatavyo:

Taratibu za vikao.

**16D.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuweka taratibu zake za kuongoza vikao na katika kutekeleza shughuli zake zikiwemo kamati za Bodi.

Kuongeza kifungu kipya cha 16E.

**17.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16E mara tu baada ya kifungu cha16D kama ifuatavyo:

Katibu wa Bodi.

**16E.**-(1) Bodi itamteuwa mwanasheria wa Mamlaka kuwa Katibu wa Bodi.

Kuongeza kifungu kipya cha 16F.

**18.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16F mara tu baada ya kifungu cha16E kama ifuatavyo:

Kazi za Katibu wa Bodi.

**16F.** Katibu atawajibika kwa Bodi na atakuwa na wajibu wa:

(a) kuchukua na kuhifadhi kwa usahihi kumbukumbu za vikao vya Bodi;

(b) kuwajuilisha wajumbe masuala yanayohusiana na Bodi;

(c) kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Bodi;

(d) kuishauri Bodi ipasavyo; na

(e) kutekeleza jambo lolote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Kuongeza kifungu kipya cha 16G.

**19.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16G mara tu baada ya kifungu cha16F kama ifuatavyo:

Kuanzishwa kwa Kamati ya Usalama Barabarani.

**16G.**-(1) Kunanzishwa Kamati ya Usalama Barabarani ambayo itaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Naibu Waziri anayeshughulikia masuala ya Usafiri Barabarani ambae atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja;

(c) Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba;

(d) Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

(e) Katibu Mkuu wa Wizara inayosimamia Usafiri Barabarani;

(f) Katibu Mkuu wa Wizara inayosimamia Elimu;

(g) Katibu Mkuu wa Wizara inayosimamia Afya;

(h) Mkuu wa Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani, Zanzibar;

(i) Mwenyekiti wa Jumuiya ya Usafiri wa Magari; na

(j) Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka.

(2) Endapo Mwenyekiti atakuwa hayupo, wajumbe waliopo watamteua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao, na mjumbe aliyechaguliwa atakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yote ya Mwenyekiti.

(3) Ukiacha wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wa Kamati watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na Bodi.

(4) Katibu wa Bodi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 16E atakuwa ni Katibu wa Kamati.

Kuongeza kifungu kipya cha 16H.

**20.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16H mara tu baada ya kifungu cha16G kama ifuatavyo:

Kazi za Kamati ya Usalama Barabarani.

**16H.**-(1) Kamati ya Usalama Barabarani itakuwa na kazi ya:

(a) kutoa elimu ya masuala ya usalama barabarani kwa jamii;

(b) kujenga uwezo wa watumiaji wa barabara kuhusiana na masuala ya usalama barabarani;

(c) kupunguza majeruhi, ulemavu na vifo vinavyasababishwa na ajali za barabarani;

(d) kupunguza upotevu wa mali unaosababishwa na ajali za barabarani;

(e) kusaidia upatikanaji wa huduma za afya za haraka baada ya ajali kutokea;

(f) kupunguza usumbufu kwa waathirika wa ajali na familia zao;

(g) kutoa picha nzuri ya Zanzibar kitaifa na kimataifa katika masuala ya usalama barabarani;

(h) kuratibu shughuli za Wiki ya Usalama Barabarani kwa Zanzibar; na

(i) kuunganisha nguvu baina ya Serikali na wahusika wa barabara ili kupungua ajali za barabarani.

Kuongeza kifungu kipya cha 16I.

**21.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16I mara tu baada ya kifungu cha 16H kama ifuatavyo:

Kamati za Bodi.

**16I.**-(1) Bodi inaweza kuanzisha kamati mbalimbali ili kurahisisha utekelezaji wa kazi zake.

(2) Taratibu, masharti na mambo mengine yanayohusiana na kamati zitakuwa kama zitakavyoelezwa na Bodi.

Kuongeza kifungu kipya cha 16J.

**22.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16J mara tu baada ya kifungu cha16I kama ifuatavyo:

Posho.

**16J.** Wajumbe wa Bodi watalipwa posho kwa mujibu wa utaratibu ulioainishwa na Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni na Miongozo yake.

Kuongeza kifungu kipya cha 16K.

**23.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16K mara tu baada ya kifungu cha16J kama ifuatavyo:

Kusita kwa ujumbe.

**16K.**-(1) Mwenyekiti au Mjumbe yeyote wa Bodi anaweza, wakati wowote, kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi na kuanzia tarehe iliyoelezwa katika taarifa hiyo au, kama tarehe haikuelezwa, kuanzia siku ambayo mamlaka ya uteuzi imepokea taarifa hiyo, atasita kuwa mjumbe wa Bodi.

(2) Pale Mwenyekiti au Mjumbe ataposita kuwa Mwenyekiti au Mjumbe wa Bodi kama itakavyokuwa, kwa sababu yoyote kabla ya muda wake wa kukaa katika nafasi hiyo kumalizika, mamlaka ya uteuzi itamteua mtu mwengine kujaza nafasi hiyo, na mtu huyo aliyeteuliwa atakaa katika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobakia cha aliyemtangulia.

Kuongeza kifungu kipya cha 16L

**24.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 16L mara tu baada ya kifungu cha16K kama ifuatavyo:

Nafasi ya Mjumbe kuwa wazi.

**16L.** Nafasi ya Mjumbe wa Bodi itakuwa wazi:

(a) akifariki;

(b) ikiwa, bila ya sababu za msingi, atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi;

(c) ikiwa atajiuzulu au kwa namna yoyote atakosa sifa ya kuwa mjumbe wa Bodi; au

(d) ikiwa atakosa uwezo kutokana na sababu za kiafya, kimwili au kiakili kutekeleza wajibu wake.

Marekebisho ya Kifungu cha 18.

**25.** Kifungu cha 18 cha Sheria Mama kinafutwa na kuandikwa kifungu kipya cha 18 kama ifuatavyo:

Kazi na uwezo wa Bodi.

**18.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 18A, Bodi itakuwa na dhamana ya usimamizi na kutoa maelekezo kwa Mamlaka na kwa madhumuni hayo, Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia uendeshaji wa Mamlaka;

(b) kumshauri Waziri katika masuala ya kisera na kimkakati ya usafiri barabarani;

(c) kupitia na kuthibitisha mipango ya utekelezaji, bajeti, taarifa na kukagua taarifa za kifedha za Mamlaka;

(d) kusimamia malengo na utendaji wa Mamlaka kama ulivyoelezwa katika:

(i) mpango wa Mwaka wa Mamlaka;

(ii) makubaliano ya Kiutendaji yoyote; na

(iii) mpango Mkakati wa Mamlaka.

(e) kutoa muongozo kwa Mkurugenzi Mkuu na watumishi wa Mamlaka;

(f) kuandaa kanuni za fedha na za wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma; na

(g) kutekeleza kazi nyengine yoyote iliyoelezwa ndani ya Sheria hii kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, Bodi katika kutekeleza kazi zake itakuwa na uwezo wa:

(a) kupendekeza kwa mamlaka husika muundo wa Taasisi na Muundo wa Utumishi wa Mamlaka.

(b) kuajiri wafanyakazi pale itakapohitajika;

(c) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi wa wafanyakazi wa Mamlaka; na

(d) kupokea na kusikiliza rufaa dhidi ya Mamlaka.

Kuongeza. kifungu kipya cha 18A.

**26.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 18A mara tu baada ya kifungu cha18 kama ifuatavyo:

Wajibu wa Waziri.

**18A-.**(1) Kwa ajili ya ufanisi na ubora katika utekelezaji wa Sheria hii, Waziri atatoa maelekezo kwa Bodi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi itawajibika kwa Waziri na italazimika:

(a) kabla ya kutekeleza maazimio yaliyoafikiwa na Bodi, kuwasilisha ripoti kwa Waziri kwa ajili ya kuthibitishwa na maelekezo;

(b) kuwasilisha ripoti ya vikao vyake vya robo mwaka; na

(c) kupokea na kusikiliza rufaa zinazotoka kwenye Bodi.

Kuongeza sehemu mpya ya XA.

**27.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza SEHEMU mpya ya XA mara tu baada ya SEHEMU X kama ifuatavyo:

## SEHEMU YA XA
## MASHARTI YA FEDHA

Kuongeza vifungu vipya.

**28.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 184-A,B,C,D na E mara tu baada ya kifungu cha 184 kama ifuatavyo:

Fedha na vyanzo vya mapato ya Mamlaka.

**184A**. Fedha na vyanzo vya mapato ya Mamlaka yatajumuisha:

(a) fedha kama zitakavyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa utaratibu wa ruzuku;

(b) michango halali, misaada, urithi au mikopo inayoweza kupokelewa kutoka kwa mtu yeyote au taasisi; na

(c) fedha nyengine zozote ambazo zinaweza kupatikana kisheria na Mamlaka.

Bajeti.

**184B.**-(1) Mamlaka, kabla ya mwaka mpya wa fedha, itaandaa bajeti ya mwaka na itaiwasilisha kwa Waziri kwa kuzingatia na kuidhinisha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(2) Waziri ataiwasilisha bajeti ya mwaka ya Mamlaka Baraza la Wawakilishi katika utaratibu na namna kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Kufungua hesabu ya Benki.

**184C**. Mamlaka itafungua hesabu ya benki kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

**Hesabu** na ukaguzi.

**184D.**-(1) Mamlaka itaweka na kuhifadhi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(2) Mkurugenzi Mkuu, kila mwisho ya mwaka wa fedha, ataandaa au ataagiza kuandaliwa:

(a) taarifa ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka huo;

(b) taarifa ya mali na madeni ya Mamlaka hadi kufikia siku ya mwisho ya mwaka wa fedha, ambayo itawasilishwa na kukaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi mwengine atakayeteuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(c) taarifa nyengine yoyote ya fedha kama ilivyoelezwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(3) Nakala za taarifa au ripoti zilizoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na nakala ya taarifa ya ukaguzi kama ipo, itawasilishwa kwa Waziri pamoja na ripoti ya utekelezaji wa kazi za Mamlaka kwa mwaka huo wa fedha, na baada ya kuipokea, Waziri ataiwasilisha Baraza la Wawakilishi.

Taarifa ya mwaka.

**184E**. Mamlaka, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, utawasilisha kwa Waziri taarifa ya mwaka inayohusiana na mwaka huo na itajumuisha:

(a) nakala za hesabu za Mamlaka zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya mkaguzi kuhusiana na hesabu hizo;

(b) taarifa ya utekelezaji dhidi ya malengo muhimu na taarifa nyengine yoyote inayohusiana nayo;

(c) taarifa kuhusiana na utendaji wa Mamlaka kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha; na

(d) taarifa nyengine yoyote kuhusiana na kazi za Mamlaka kama Waziri atakavyohitaji.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 2 Disemba, 2019.

..............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***